Mpango wa serikali kusambaza umeme vijijini wazidi kutanuka kwa kasi

Ngeleja awaita jou wawekezaji 'uchwara' wanaoficha siri zao

NA ANGELA SEBASTIAN

TANGU kuingia kwa mfumo wa soko huria nchini kumekuwa na vilio vya wazawa juu ya soko la bidhaa za ndani kutekwa na bidhaa za kigeni na matokeo yake kukwamisha juhudi zao za kujikwamua kiuchumi.

Hali hiyo imeambatana na kuongezeka kwa wimbi la wawekezaji ambalo limeteka fursa za kiuchumi za wazawa na kuwafanya wengeji kuwa vibarua.

Pamoja na kuwepo kwa wawekezaji hao, baadhi yao wamejigeuza mlungu watu kwa kuwanyanyasa na kuwadharau wazawa na kutaka kuwatumia kwa kadri watakavyo ili kujinufaisha zaidi.

Kutokana na hali hiyo, Waziri na Nishati na Madini, William Ngeleja(pichani), ili kukabiliana na ukiukwaji wa haki za msingi za raia zinazofanywa na baadhi ya wawekezaji, wizara yake imeweka mikakati ili kuondoa kero mbalimbali zinazofanywa na wadau hao wa maendeleo.

Akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kagera hivi karibuni, kukagua miradi ya umeme inayotekelezwa kwa udhamini wa seriklia kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Ngeleja alionya kuwa serikali haitasita kuchukua hatua kulinda raia wake dhidi ya wawekezaji wakorofi.

Alipokutana na wafanyakazi wa mgodi ya Kabanda na Tulawaka alisema Tanzania inahitaji wawekezaji wenye nia njema, wanaofuata taratibu na kuweka mambo yao wazi ikiwa ni pamoja na kuleta maendeleo ya nchi na mwananchi mmoja mmoja.

Alieleza kuwa serikali haitamvumilia mwekezaji ambaye hatatekeleza masharti na sheria zilizopo.

"Kwa sasa sheria ya uwekezaji nchini hasa kwa upande wa madini inantaka kila anayewekeza kuhakikisha ajira anayotoa kwanza ilenge Watanzania, hasa wale wanaozunguka migodi ili kuonda matatizo ya uvamizi na mapigano yanayoweza kujitokeza kati ya wananchi na wawekezaji," alisema Ngeleja.

Mmoja wa wafanyakazi wa mgodi wa Tulawaka ulioko wilayani Biharamulo, Alex Ndalo, ambaye hufanya kazi katika kitengo cha umeme kwa niaba ya wafanyakazi wazawa wa mgodi huo, alimweleza Ngeleja kuwa kumekuwa na vitendo vya unyanyasaji vinavyofanywa na uongozi wa mgodi huo.

Ndalo alisema wanawashauri viongozi waandamizi wa serikali akiwemo waziri wa nishati na madini kufanya ziara kutembelea migodi hiyo mara kwa mara ili kujionea unyanyasaji huo.

"Watumishi wazawa tuna mambo mengi ya kueleza lakini hatujawaona viongozi husika ili tuwafahamishe ukweli wa mambo, hata wengine wakija tukiwaeleza halona anayekubali kuwasema wawekezaji mbele yetu ili wayatolee majibu malalamiko yetu. Wakati mwingine tunekuwa tukifikia hatua ya kusema kuwa labda viongozi wetu wanahongwa na wawekezaji ili tuendelee kunnia tukiwa nchini mwetu," alieleza

Alisema wafanyakazi wazawa katika mgodi wa Tulawaka wanalalamikia uongozi wa mgodi huo kwa kuwatenga, ambapo wazawa hutumia bwalo la chakula tofauti na wageni hata vyakula wanavyokula vinakuwa tofauti kulingana na cheo cha mtu.

Alieleza kwamba chakula kinachaliwa na wenye vyeo ni bora zaidi ya wale wasiokuwa na vyeo, jambo ambalo wamedai ni unyanyasaji kwani kama wanafanyakazi kwenye kampuni moja, kwanini wasitumie bwalo moja ?

Aliataja unyanyasaji mwingine kuwa ni wazawa kulipwa ujira mdogo kulinganisha na kazi ngumu wanazofanya. Kwa mujibu wa Ndalo, wafanyakazi wazawa wanalipwa asilimia saba mpaka tisa ya mshahara wa wafanyakazi wa kigeni.

Kaimu Meneja wa mgodi wa Tulawaka, Eric Acheampang ambaye ni raia wa Ghana, alisema mishahara inayotolewa na Tulawaka ni kiwango kile kile kinachotolewa kwa wafanyakazi wengine wahoko katika migodi yote inayomilikiwa na Kampuni mama ya Barrick, kwenye migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na North Mara.

Kwa mujibu wa Acheampang, mishahara hiyo imepangwa na bodi ya wakurugenzi. Pia alieleza kwamba wafanyakazi hao kupitia chama chao na uongozi wa mgodi wameishakaa na kujadili namna ya kutumia bwalo moja badala ya kutengana.

Acheampang akisema taarifa ya miradi wa uchimbaji madini kwa Waziri Ngeleja alisema mgodi huo hutoa misaada mingi kwa jamii lakini hakutaja ni kiasi gani cha fedha walichotumia kuchangia huduma hizo za jamii.

Pia, wawekezaji hao hawakuonyesha ni kiasi gani wametumia kuwekeza na lini wameudisha gharama zao na kuanza kulipa mapato, kitu ambacho kilimshangaza Waziri Ngeleja.

NGELEJA ASHANGAA

Kutokana na upungufu huo, Waziri Ngeleja alikataa na kueleza, "Taarifa hii siipokei ina mapungufu mengi, nilitarajia kuwa utaeleza mambo mengi ya msingi, unaeleza mnasaidia jamii lakini hutaji ni kiasi gani cha pesa milichotumia, huelezi mnazalisha nini, lini mmeanza kulipa kodi, lini mmerudisha gharama zenu, tumekuja kazini tunahitaji kuelezwa mambo ya msingi, unaeleza eti tumechangia 'graduation' hayo si mambo ya kutueleza, kwanini mnataka kusema kwa kificho, mnataka serikali iwasemee?

"Hatutakubali kuwalinda wawekezaji wanaotaka kuichonganisha serikali na wananchi wake, hatuji hapa koimbiwa shairi, tunakuja ili kila kitu kiwekwe wazi ili wananchi waweze kuelewa kupitia vyombo vya habari. Wawekezaji wa aina hii wanaofanya kazi kwa kificho hatutawavumilia na hatuwahitaji," aliongeza Ngeleja

Ngeleja aliomba wizara ya kazi na ajira, idara ya mambo ya ndani kupitia idara ya uhamiaji kwa kushirikiana na wizara ya nishati na madini kutembelea migodi mara kwa mara ili kubaini kero za wafanyakazi na kuzitafutia ufumbuzi ikiwa pamoja na kuangalia utaratubu unaotumika kwa wafanyakazi wageni kuingia nchi na kupata ajira migodini.

Alisema baadhi ya wawekezaji wa migodi nchini wamekuwa na uhusiano mbaya na jamii inayowazunguka. Kwa sasa sera ya madini inaeleza kwamba mgodi wowote utakapofungulwa lazima serikali iwe na hisa, ambapo kila mgodi umeagizwa kupeleka taarifa wizara ya nishati na madini inayoonyesha Watanzania wangapi wamepewa nafasi ya kutoa huduma katika migodi hiyo .

MCHANGO WA SEKTA YA MADINI

Ngeleja alisema kwamba mchango unaotolewa na sekta ya madini husaidia kuongeza mapato, hivyo kusaidia huduma mbalimbali za jamii kama vile ununuzi wa dawa katika hospitali, ununuzi wa vitabu shuleni, na utengenezaji wa barabara.

Aliwashauri wananchi kuwapunza watu wanaoeleza kuwa serikali imekuwa ikopata asilimia tatu kwenye madini na mwekezaji anapata asilimi 97, ambapo alisema huo ni upotoshaji wa kisiasa wala sio wa kitaalam.

Akitoa mfano wa mgodi wa Tulawaka, alieleza kuwa kuanzia mwaka huu watalipia zaidi ya sh.bilioni 50 kwa mwaka, mishahara ya wafanyakazi hukatwa kodi ya asilimia 14 hadi 30 na huingia serikalini, kuendeleza ufundi wanalipia asilimia sita , kodi ya zuio asilimia tatu, stampu asilimi moja na mrahaba wanalipia asilimia nne.

Kwa mantiki hiyo, Ngeleja alisema wanaopotosha ukweli wa kinachochangiwa na sekta ya madini wanafanya hivyo kwa malengo ya siasa na wanasukuawa na mihemko isiyozingatia utalaam.

Pia, aliwataka wananchi wanaozunguka migodi hiyo kuzalisha bidhaa mbalimbali zenye ubora ili wawekezaji waweze kutumia bidhaa za Tanzania ili kuinua vipato vyao.

UMEME VIJIJINI

Akiwa wilaya za Karagwe na Bukoba Vijijini kutembelea miradi wa kusambaza umeme vijijini unaofadhiliwa na serikali ya Tanzania kwa asilimia 100, alisema huo ni mkakati wa Chama Cha Mapinduzi ili kuwapatia umeme wananchi vijijini.

Alisema serikali imekuwa ikitafuta njia mbalimbali za kupunguza gharama za umeme kwa wananchi ambapo mwaka jana, ilianzisha miradi wa majaribio katika wilaya mbili za Tanzania ambazo ni Mbozi na Kilombero.

Mradi huo utagharimu sh.bilioni 16 pindi utakapokamilika na utakuwa mkombozi kwa wananchi vijijini, hivyo kuwezesha idadi ya watumiaji umeme kufikia asilimia 30 ya Watanzani wote tofauti na sasa ambapo ni asilimia 17.

Alisema mpango wa sasa wa taifa ni kuhakikisha mikoa nchini inaingizwa katika gridi ya taifa mradi wa kuzalisha gesi na makaa ya mawe inayotarajiwa kukamilika mwakani na kuingiza megawati 300 za umeme.

"Pia upo mradi utakaodhaminiwa na Tanzania kwa kushirikiana na nchi Brazil ambapo tumeishatiliana saini na utakamilika baada ya miaka minne na nusu na utazalisha megawati 2,100," alisema Ngeleja.

Ngeleja aliliagiza Shirika la Umeme nchini (TANESCO) mkoa wa Kagera kuhakikisha wanakamilisha mradi wa umeme utakaogharimu sh. milioni 250, ambao umechukua muda mrefu tangu uanzishwe mwaka 2004 bila kukamilika.

Mradi huo upo katika Kata ya Rwambaizi, wilayani Karagwe ambapo wananchi wamedai hata nguze zimeanza kuhamishwa na kupelekwa sehemu nyingine.

Aliwataka REA kuhakikisha wanaingiza Kata ya Rulenge iliyoko wilayani Ngara kwenye mradi wa kupata umeme wa megawat 30 zinazohitajika hivi sasa. Mradi huo utagharimu sh. milioni 630 mpaka kukamilika kwake.

Kaimu Meneja wa TANESCO, mkoani Kagera, Ramadhani Minge alisema mradi wa umeme vijijini unaotekelezwa katika wilaya za Bukoba Vijijini na Karagwe unatarajiwa kukamilika Mei, mwaka huu ■